

MWONGOZO WA SUALA LA KUTAFSIRI NCHINI TANZANIA

A. S. NCHIMBI*

1. Kwa watu wengi, neno hili la TAFSIRI ni la kawaida katika mazungumzo yao ya kila siku. Maana inayoeleweka na kukubalika na wengi wetu ya neno hili TAFSIRI—ni ile ya kutoa “*maana*” ya *habari fulani* “Maana” hiyo inaweza ama kutolewa katika maneno ya lugha ile ile (L_1) ya habari ambayo inatarajiwa kutafsiriwa: $(t = m + a)$,¹ ama katika lugha tofauti (L_2) na ile (L_1) ya habari yenyewe inayotarajiwa kutafsiriwa: $(t \xrightarrow{\text{---}} m^1 + a^1)$ ²

Wana-Isimu wa siku hizi wamekubaliana kwamba hapana uwezekano wa “kuitafsiri habari fulani” iliyoandikwa katika lugha L_1 katika lugha K_2 kwa asilimia ‘mia moja taslim.’ Maadam TAFSIRI inamhitaji anayetafsiri kufahamu barabara habari yenyewe inayotarajiwa kutafsiriwa, yaani L_1 na pia kuifahamu barabara miundo mbali mbali ya lugha L_2 ambamo TAFSIRI hiyo itafanyika, ni dhahiri kwamba aina yo yote ya TAFSIRI lazima ifanyike katika lugha ambayo anayetafsiri awe amezaliwa nayo. Zaidi ya hayo, mambo ambayo yanasaidia kuifanya TAFSIRI yo yote iwe sahihi zaidi ni elimu ya mfasiri katika utamaduni, siasa na mazingira ya nchi ambamo lugha zinazotumika katika TAFSIRI hiyo zimekomazwa.³

2. Kwa nini TAFSIRI ni muhimu katika maisha yetu ya kila siku? Swali hili ni muhimu sana, kwani tusipofafanua umaarufu wa TAFSIRI katika maisha yetu ya kila siku, basi ni halali pia kusahau suala la TAFSIRI. Lakini ukweli ni kwamba maisha yetu daima hujitafsiri kufuatana na utamaduni wetu, siasa yetu na mazingira yetu. Kwa hiyo, suala la TAFSIRI ni la faradhi katika maisha ya binadamu. Kwa mfano, ni sisi Watanzania pekee tunaoweza kuhisi jinsi gani siasa ya Ujamaa na Kujitegemea inavyoweza kususukuma mbele kwa haraka kimaendeleo kutokana na utamaduni wetu, ujuzi wetu wa siasa zingine mbali mbali, na mazingira ya nchi yetu yalivyo. Kutokana na hisi zetu katika mambo hayo mbali mbali ambayo yanafanya sehemu muhimu ya ubinadamu wetu, ndipo tutakapoweza kutoa TAFSIRI iliyo sahihi kabisa; kwani lugha pekee ndiyo inayoweza kueleza hisi hizo katika mambo hayo mbali mbali. Kwa hiyo, ni dhahiri kwamba mfasiri anayetumia lugha mbili ambazo kwake yeye ni za kigeni tupu, aghalabu hutoa TAFSIRI zilizo sahihi.

3. Ni matumaini yetu kwamba cho chote wanachofanya Watanzania hapa makwao au katika nchi za ng'ambo, lazima kiwe kwa manufaa ya Watanzania wenyewe; na hasa kwa manufaa ya wale waishio nyumbani, Tanzania. Ni tegemeo letu pia kwamba wafanyakazi wa kigeni hapa nchini katika kutekeleza

*A. S. Nchimbi is an assistant lecturer in the Department of Languages and Linguistics, University of Dar es Salaam.

wajibu wa kazi zao, lazima uwe katika kulifikia lengo hilo hilo, yaani “kwa ajili ya manufaa ya Watanzania wenyewe.”

4. Lugha itumiwayo na Watanzania wengi hapa nchini katika utatuzi wa vikwazo mbali mbali vinavyowakabili katika maisha yao ya kila siku ni KISWAHILI ambacho msamiati wake ni mchanganyiko wa maneno mbali mbali ya vijilugha vyote vya hapa nchini vyenye asili ya Kibantu. Zaidi ya hapo, kuna maneno mengine pia yaliyojiingiza katika KISWAHILI yenye asili ya lugha za Watawala wetu wa Kikoloni; kama vile maneno yenye asili ya Kiarabu, Kireno, Kifaransa, Kijerumani, Kiingereza, n.k. Sarufi ya Kiswahili ni ya kibantu kitupu. Kwa Watanzania, KISWAHILI ni lugha yao ya Taifa tangu mwaka 1968. Ingawaje uamuzi huu ulichelewa kutamkwa rasmi na serikali, ukweli ni kwamba, kwa muda wa karne nyingi, KISWAHILI kimejidhihirisha kwa Watanzania wengi, kwamba ndiyo lugha pekee ambayo wameitumia katika mawasiliano tangu enzi hizo mpaka leo katika maisha yao ya kila siku.

5. Tangu mwanzo wa karne hii ya ishirini, Watanzania tumeonyesha ari ya kutaka kujifunza lugha za kigeni; sio zile tu za waliokuwa Watawala wetu wa Kikoloni, kama vile Kiarabu, Kijerumani na Kiingereza, bali pia Kifaransa, Kireno, Kirusi, na nyingi nyinginezo. Kwa hivi sasa, lugha rasmi za kigeni ambazo Watanzania tunajifunza kusema na kuandika kwa ufasaha ni Kiingereza na Kifaransa; nazo hufundishwa katika mashule yetu ya hapa nchini kwa idhini ya serikali ya Wananchi wenyewe. Si ajabu kwamba serikali ya Wananchi huenda ikaamua kuongeza ufundishaji wa lugha zingine za kigeni katika mashule yetu hapa nchini hapo baadaye, kama vile Kireno, Kichina, Kijerumani n.k.

6. Mara nyingi, Watanzania wanapoamua jambo fulani kwa njia ya serikali yao huwa wana sababu mahsus. Sababu ya uamuzi wa serikali ya Tanzania wa kukifanya *Kiswahili kuwa Lugha ya Taifa* ni kwamba lugha hii, kama ilivyosemwa hapo awali, ni lugha ya mawasiliano baina ya Watanzania; zaidi ya hayo, Kiswahili ni sehemu muhimu ya utu wa Mtanzania kwani ndiyo lugha pekee anayoweza kuitumia kueleza kinaganaga utamaduni wake, siasa yake na mazingira ya nchi yake huyo Mtanzania. Hivi leo, Kiswahili kinatumika katika kufundishia masomo mbali mbali ya Fani na Sayansi katika shule nyingi na vyuo vingi nchini.

Kiingereza na Kifaransa hufundishwa kama lugha za kigeni hapa nchini. Moja wapo ya sababu muhimu zilizopendekezwa na wananchi katika kuamua ufundishaji wa lugha mbili hizi za kigeni hapa nchini, ni kwamba lugha mbili hizi hutumiwa na watu wengi hapa duniani ambao kimaisha wanatuhusu sana; kwa mfano, tunaendelea kujifunza Kiingereza kwa sababu Waingereza bado tunahusiana nao. Tunajifunza Kifaransa kwa sababu kuna Waafrika watumiao lugha ya Kifaransa na ambao tunahusiana nao sio katika Uafrika tu, bali pia katika uendeshaji wa vita vyetu vya kulikomboa bara letu la Afrika kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni. Kiwe Kiswahili au Kiingereza, Kifaransa au Kireno, n.k. tunajifunza lugha hizi ili pawepo na mawasiliano ya hali ya juu baina yetu sisi Waswahili na hao wenzetu watumiao lugha zingine wakati tunapokabiliwa

UTAFITI

na tatizo linalotuhusu wote katika jumuiya yetu. Mataifa ambayo huhusiana katika usawa wa matatizo yao lakini ambayo yanatofautiana katika lugha, hayana budi kuanzisha madarasa ya kuwafundisha wananchi wake lugha zinazowahusu. Kwa mfano, iwapo sisi Watanzania tuna uhusiano wa aina fulani na Wachina, uhusiano ambao utasababisha pande zote mbili hizi kuonana mara kwa mara katika jitihada zetu za kutatua tatizo fulani linalotukabili, basi hapana budi serikali ya Watanzania iamue kuanzisha madarasa ya kufundishia wananchi wake lugha ya KICHINA. Hali kadhalika, serikali ya Wachina itabidi iamue kuanzisha madarasa ya kufundishia wananchi wake lugha ya Watanzania, yaani KISWAHILI. Iwapo nadharia kama hii ingedhihirishwa kimatendo tangu miaka mingi iliyopita kati yetu sisi Watanzania na Wachina, TAFSIRI ambayo ingetumika wakati wa mikutano mbali mbali ya Wakuu wa serikali za mataifa hayo mawili katika jitihada zao za kutafuta jawabu la swala linalowakabili ingekuwa imechukua sura kama ifuatayo:

I. Kwa upande wa Wachina:

KISWAHILI \longrightarrow KICHINA
(Lugha ya kigeni) (Lugha ya kwao)

(Mchina aliye hodari katika Kiswahili na aliyefuzu utaalamu wa kutafsiri atahitajika kumtafsiria katika Kichina Mkuu wa serikali yake yale yasemwayo kwa Kiswahili na Mkuu wa serikali ya Watanzania katika mkutano huo).

II. Kwa upande wa Watanzania:

KICHINA \longrightarrow KISWAHILI
(Lugha ya kigeni) (Lugha ya kwetu)

(Mtanzania aliye hodari katika Kichina na aliyefuzu utaalamu wa kutafsiri atahitajika kumtafsiria katika Kiswahili Mkuu wa serikali yetu yale yasemwayo kwa Kichina na Mkuu wa serikali ya Wachina katika mkutano huo).

7. Ni dhahiri kwamba kama pangukuwa na haja, *Mwalimu-Mtaalamu* wa Kichina wa kutafsiri *Kiswahili* katika *Kichina* angeweza kuajiriwa na serikali ya Watanzania ili nasi pia tuupate utaalamu wa kuitoa tafsiri iliyo sahihi zaidi yenye sura kama ifuatavyo:

III. KISWAHILI \longrightarrow KICHINA
(Lugha ya kwetu) (Lugha ya kigeni)


Hali kadhalika, *Mwalimu Mtaalamu* wa Kitanzania wa kutafsiri *Kichina* katika *Kiswahili* angeweza kuajiriwa na serikali ya Wachina ili nao pia wapate utaalamu wa kuitoa tafsiri iliyo sahihi zaidi yenye sura kama ifuatavyo:

IV. KICHINA \longleftrightarrow KISWAHILI
(Lugha ya kwao) (Lugha ya kwetu)

Ndiyo kusema kwamba katika nchi hizi mbili tungeshuhudia kuwepo kwa madarasa yanayofundisha wananchi wake tafsiri zenye sura mbili, kama zifuatazo:

(a) Kwa sisi Watanzania, sura za TAFSIRI zetu zingekuwa kama zifuatazo:

V. KICHINA \longleftrightarrow KISWAHILI



*Ukweli ni kwamba kita Taifa lingenda juu na Wataalamu-Wananchi wake ambao wangehusika na UFAANUZI WA HALI YA JUU na hatimaye kurika TAFSIRI iliyoyo SAHIMI KABISA juu ya TATIZO linalokabiri MATAIFA. Ili lengo hili liweze kueleweka vilivyo, hapana budi TAIFA linalohusika na TATIZO hilo LIJIELEZE katika LUGHA YA WANANCHI WAKE wakati wa kupeswa MAWAZO YA HALI YA JUU.

UTAFITI

(b) Kwa wenzetu Wachina, sura za TAFSIRI zao zingekuwa kama zifuazo:

VI. KISWAHILI ←————→ KICHINA

8. Ni lazima ikumbukwe daima kwamba MTU BINAFSI ana namna yake pekee ya kufafanua jambo fulani katika jitihada yake ya kulitafsiri jambo hilo kwa uwezo wake wote; TAIFA nalo pia, lina msimamo wake katika ufafanuzi wa jambo fulani ili kulitafsiri jambo hilo kwa usahihi wa hali ya juu liwezavyo; JUMUIA NDOGO YA MATAIFA HURU, nayo pia, ina msimamo wake mahsusi ambao huenda ukawa tofauti na ule wa MTU BINAFSI au wa TAIFA fulani katika ufafanuzi wa jambo fulani ili kulitafsiri jambo hilo kwa usahihi wa hali ya juu iwezavyo. Ili pawepo na uwezekano wa kufafanua jambo fulani katika jitihada ya kulitafsiri jambo hilo kwa usahihi wa hali ya juu iwezekanavyo, anayehusika na ufafanuzi huo wa hali ya juu na hatimaye kuifikia tafsiri iliyo sahihi kabisa, hana budi kutumia ujuzi wake wote wa (i) utamaduni wa Taifa lake, (ii) siasa ya Taifa lake, na (iii) mazingira ya nchi yake yote. Kwa hiyo, katika kupeana mawazo juu ya tatizo fulani linalokabili MATAIFA mawili ambayo yamepania kumaliza tatizo hilo, lazima kila TAIFA, kwa upande wake, litumie lugha ya Wananchi wake katika kujieleza bila wasi wasi kifikra kuliko kuwa katika hali ya juu. Twaweza kufafanua zaidi haya yaliyosemwa hapo juu. Twaweza kufafanua zaidi hayo yaliyosemwa juu kwa msaada wa mchoro ufuatao:

9. Mabwana zetu Waingereza (na hata baadhi ya Watanzania wenzetu waliolewa kasumba ya kusema na kuandika lugha ya Kiingereza) wangependa kuona kwamba habari zinazosemwa au zilizoandikwa katika lugha zingine zote zitafsiriwe katika lugha ya Mabwana zetu Waingereza—yaani Kiingereza. Kwa hiyo, sura za utumiaji wa lugha mbali mbali katika Tanzania wangependa zive kama zifuatazo:


(i) Katika mawasiliano ya aina yo yote kati ya Watanzania wenyewe kwa wenyewe, sura ya utumiaji wa lugha ingekuwa kama ifuatayo:


Kiswahili ←————→ Kiingereza

au

Kiingereza ←————→ Kiingereza

(ii) Katika mawasiliano kati ya Watanzania na watu wa mataifa mengine, sura ya utumiaji wa lugha mbali mbali katika Tanzania ingekuwa kama ifuatayo:





Jibu linalotoka kwa Watanzania kwenda kwa mataifa hayo wangependa liwe kwa Kiingereza.

Lakini tukichunguza sana mpango huu wa matumizi ya lugha hizi, tutaona kwamba kuna mushkeli mahali fulani. Kwa mfano:

(a) Ni dhahiri kwamba Watanzania hawajui Kifaransa, lakini Waingereza wengi wanajua Kifaransa. Iwapo tatizo lilikuwa linawahusu *Watanzania* na *Wafaransa*, basi Taifa la Tanzania lingelazimika kuajiri Wataalamu wa Kiingereza wa kutafsiri *Kifaransa* katika *Kiingereza*. Na iwapo tatizo hilo lingekuwa la kudumu, basi haja ya kuwaajiri Wataalamu-Waingereza ingekuwa ya kudumu pia. Ni dhahiri kwamba, hii ni njia mojawapo ya sisi wanyonge kujiona *tunalazimika kumpa kazi* Mwingereza. Na Waingereza, kwa upande wao, wangeweza kutumia mbinu kadha wa kadha ili kuudumisha unyonge wetu huo wa kujiona kwamba *tunalazimika kumuajiri* kila mara yeye tu katika kazi za aina hii. Kwa hiyo iwapo Watanzania walio wengi wangependa kuarifiwa mambo yaliyozungumzwa kati ya Wakuu wa serikali ya Wafaransa na Wakuu wa serikali yetu, Wakuu wa serikali yetu ingewabidi wapate TAFSIRI ya habari iliyoandikwa au iliyosemwa kwa Kifaransa katika Kiingereza kwanza, halafu apatikane Mtaalamu mwingine wa kutafsiri tafsiri hii ya Kiingereza katika Kiswahili, lugha ambayo sasa itumike kuwarifu Watanzania wote kwa njia ya magazeti na taarifa za habari za Idhaa ya Redio, Tanzania. Twaweza kuionyesha sura ya mfano huu wa matumizi ya lugha hapa Tanzania kama hii ifuatayo:

(b) Mwanachuo Mtanzania wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam anayeamua kuchukua *tafsiri* inayohusu lugha za Kiingereza na Kifaransa—(Kiingereza \longleftrightarrow Kifaransa) yu katika mkondo wa kuzishughulikia lugha mbili zilizo ngeni kwake kwa kila hali. *KITAMADUNI* hapana lugha hata moja kati ya hizo mbili inayoweza kueleza kinaganaga hisi zetu; *KIJIJOGRAFIA*, lugha zote mbili hizi zimetoka mbali sana na Tanzania—yaani, Uingereza na Ufaransa. Kwa hiyo, mazingira ambamo lugha mbili hizi zimekomaa ni mageni pia kwa Mwanachuo-Mtanzania. Mtindo wa SIASA ya Waingereza na Wafaransa ni tofauti na huu wetu sisi Watanzania: Kiingereza na Kifaransa ni lugha zilizokomazwa, na zinaendelea kukomazwa zaidi, katika SIASA ya kibepari. Mwanachuo-Mtanzania anakomazwa katika SIASA ya Ujamaa na Kujitegemea iliyofanana sana na mila za kabila lake.

Lakini kwa upande mwingine, tafsiri hii hii inayohusu lugha za Kiingereza na Kifaransa—(Kiingereza \longleftrightarrow Kifaransa) *si ngeni* kwa hali yo yote kwa Mwanachuo-Mwingereza au Mwanachuo-Mfaransa kwa sababu ambazo ni dhahiri. Kwa hiyo, ukweli ni kwamba Mwanachuo-Mtanzania wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam anapotahiniwa juu ya tafsiri ya habari inayohusu lugha ya Kiingereza na Kifaransa, itambidi *ajitahidi mara dufu zaidi* kuliko Mwanachuo-Mwingereza za wa Chuo Kikuu cha Landani au Mwanachuo-Mfaransa wa Chuo Kikuu cha Parisi kama nao hao wange

tahimiwa juu ya tafsiri ya habari hiyo ili matokeo yao ya mwisho, baada ya masahihisho ya mitihani yao, yastahili, kama alama ya asili-mia arobaini (40%). Kwa Mwanachuo-Mwingereza au Mwanachuo-Mfaransa, tafsiri ya aina hii, yaani—Kiingereza \leftarrow \longrightarrow Kifaransa, ni ya kawaida kwake; kwani lugha mojawapo ya hizo mbili, kwake ni ya kuzaliwa nayo. Kwa hiyo, alikuwa amefanya mtihani wa kutafsiri *lugha ya kigeni* katika *lugha ya kwake*. Na apewapo alama ya asili-mia arobaini (40%) kwa kazi yake, walimwengu wake watamweka mahali pake katika kusifiwa; yaani, kama ni HODARI au HODARI WA WASTANI au HAFAI kwa *kutafsiri*. Kwa kawaida ya Vyuo Vikuu mbali mbali vya ulimwengu, alama ya asili-mia arobaini (40%=C) inastahili sifa hii: HODARI WA WASTANI.

Mwanachuo-Mtanzania aliyepata alama ya asili-mia arobaini (40%), atawekwa mahali gani kisifa na walimwengu wake? Akumbuke kwamba mtahiniwa huyu *ilimbidi* ajifunze kwanza lugha mbili hizi, yaani Kiingereza na Kifaransa, kabla ya kujifunza *isimu* yake na hatimaye kuitumia elimu hiyo katika majaribio ya kiutalaamu, kama mitihani hii ya *kutafsiri*. Mtahiniwa mwenzake Mwanachuo-Mwingereza au Mwanachuo-Mfaransa *hakuwa na haja* ya kujifunza kwanza lugha yake hapo chuoni pake kwa sababu lugha hiyo amezaliwa nayo; yeye alianza kujifunza moja kwa moja *isimu* ya lugha yake na utaalumu wa kuitafsiri lugha yake katika lugha ya kigeni kwa muda wake wote alioishi hapo chuoni pake. Mara nyingi Vyuo Vikuu mbali mbali vya ulimwengu vimetumia *wembe ule ule*—yaani alama ya asili-mia arobaini (40%=C) istahili sifa ya: HODARI WA WASTANI, Uamuzi huu ni *sawa*: lakini matokeo yake ni mabaya kwa upande wa Mwanachuo-Mtanzania. Ukweli ni kwamba kwa Mwanachuo-Mtanzania anayestahili alama ya asili-mia arobaini (40%=C) ana *akili zaidi* kuliko Mwanachuo-Mwingereza au Mwanachuo-Mfaransa anayestahili alama ya asili-mia arobaini (40%=C) katika mtihani huo wa kutafsiri Kiingereza \leftarrow \longrightarrow Kifaransa. Yaani, Mwanachuo-Mtanzania aliyestahili kupata alama ya asili-mia arobaini (40%=C) *ingebidi alingane* na Mwanachuo-Mwingereza au Mwanachuo-Mfaransa aliyestahili kupata alama ya asili-mia, kama hamsini na tano (55%=B). Hii ina maana kwamba *juhudi* ambazo tungetegemea Mwanachuo-Mtanzania (40%) kuzionyesha katika utekelezaji wa wajibu wake wa kazi za Wizara au Shirika lililomwajiri ingelingana na ile *juhudi* ya Mwanachuo-Mwingereza au Mwanachuo-Mfaransa (55%).

Lakini kwa sababu ya unyonge wetu, tunalazimika kumtukuza Mwanachuo-Mwingereza (40%=C) au Mwanachuo-Mfaransa (40%=C) kwa kumtunukia sifa ya Mwanachuo-Mtanzania wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam anayestahili sifa ya alama ya asili-mia (55%=), yaani, HODARI.

Unyonge huu wa TAIFA la Watanzania kujiona kwamba wanalazimika kumwajiri Mwingereza, eti kwa sababu ya ujuzi wa lugha yake ya Kiingereza na nyinginezo za huko Ulaya, kutufanyia kazi ya kutafsiri habari yo yote itokapo papa hapa nchini au nchi za nje, waweza kupigwa vita, na unyonge

UTAFITI

wetu huo kutoweka kabisa katika TAIFA letu, iwapo tu, tukikubaliana kushirikiana katika utekelezaji wa mambo haya yafuatayo:

- I. Sisi Watanzania tukatae kuamini kwamba ni lugha ya Kiingereza *tu* inayoweza kueleza utamaduni, siasa na mazingira ya binadamu kote ulimwenguni na kwamba lugha zingine, lugha yetu tukufu ya Kiswahili ikiwa mojawapo haziwezi kufanya hivyo.
 - II. Sisi Watanzania tujenge imani kwamba lugha yo yote ya binadamu katika taifa lake imejikamilisha yenyewe katika kueleza vilivyo utamaduni, siasa na mazingira ya binadamu wa taifa hilo kuliko lugha nyingine yo yote ya bandia.
 - III. TANU na vyombo vyake, vizidi kutoa uamuzi wa busara wa kimapinduzi katika jitihada yake ya kukomboa wananchi wake. Kwa mfano, izidi kutoa uamuzi wa kutumia lugha ya Kiswahili katika ufundishaji wa masomo yote ya shule za hapa nchini, kufuatana na *hali ilivyo* katika shule hizo.
 - IV. Sisi Watanzania tusiwe chanzo cha kuwepo kwa hali ambayo inaweza kusababisha uzorotaji katika kutekeleza jambo Namba III hapo juu. Ili uepukane na sifa mbaya kama hii, itakubidi, na hasa ukiwa kama Kiongozi wa wenzako hapo kazini au hapo uishipo, kuwahoji wenzako juu ya njia mbali mbali ambazo zingesaidea kutatua vikwazo vya hapo kazini au kijijini penu.
 - V. Sisi Watanzania tuwe macho kugundua hila zo zote za wageni za kutaka kuunyonya utaalamu wetu katika utamaduni wetu, siasa na mazingira yetu.
 - VI. Kutokana na yale tunayoyashuhudia yanatokea mwaka hata mwaka katika taifa letu; sisi Watanzania tunaamini kwamba taifa letu linaendelea. Tunaposema kwamba taifa linaendelea, tunamaanisha kwamba binadamu wa taifa hili wanaendelea; na kuendelea kwa binadamu ni kuendelea kwa utamaduni wake, siasa yake na mazingira yake pamoja. Lugha pekee ya binadamu wa taifa lo lote ndiyo itakayoweza kueleza maendeleo hayo katika daraja mbali mbali zilizotajwa hapo juu. Kwa sisi Watanzania, lugha iliyo na jukumu kama hili ni Kiswahili.
 - VII. Sisi Watanzania, tujenge moyo wa kutafutatafuta msamiati wa kitaalamu katika mambo mbali mbali yanayotuhusu. Tufundishane msamiati huo ili tuutumie vilivyo katika mawasiliano yanayotuhusu.
10. Kwa kuwa KISWAHILI ndiyo lugha ya Taifa la Watanzania wanaoendelea mwaka hata mwaka kiutamaduni, kisiasa na kimazingira, ninapenda sura za matumizi ya lugha hapa nchini ziwe kama zifuatazo:
- (i) Katika mawasiliano kati ya Watanzania wenyewe kwa wenyewe:
Kiswahili \longleftrightarrow Kiswahili.
 - (ii) Katika mawasiliano kati ya Taifa la Watanzania na Mataifa mengine:

Hapana budi tukumbuke pia, kwamba iwapo Watanzania tutatilia mkazo zaidi katika TAFSIRI zinazohusu KISWAHILI na lugha yo yote yenye asili

Lugha ya Kigeni \longleftrightarrow Kiswahili

Kwa mfano:

- (a) Kikamba \longleftrightarrow Kiswahili
- (b) Kiingereza \longleftrightarrow Kiswahili
- (c) Kiarabu \longleftrightarrow Kiswahili
- (d) Kilingala \longleftrightarrow Kiswahili
- (e) Kifaransa \longleftrightarrow Kiswahili
- (f) Kiwolofu \longleftrightarrow Kiswahili
- (g) Kiurdu \longleftrightarrow Kiswahili
- (h) Kihausa \longleftrightarrow Kiswahili
- (i) Kireno \longleftrightarrow Kiswahili
- (j) Kichina \longleftrightarrow Kiswahili

ya Mwafrika, tutakuwa tunauendeleza sio utaalamu wetu katika kutafsiri tu, bali pia utamaduni wa Mwafrika, siasa ya Mwafrika, mazingira ya Mwafrika na hasa lugha ya Mwafrika.

FOOTNOTES

1. ambapo: (t, m, a, \longleftrightarrow) = L_1
2. (t, m', a', \longleftrightarrow) = L_2
3. Kutokana na yaliyomo katika kitabu kiiwacho: "Language-Teaching Abstracts", Volume 7, No. 3, July, 1974).
4. Neno hili *Mabwana* (wengi) *Bwana* (mmoja), linaonyesha kwamba kati ya wale wanaolitumia, mmoja wao ni mtwana. Siku hizi, Watanzania hutumia neno *Ndugu*.

SUMMARY

THE RATIONALE OF TRANSLATION IN TANZANIA

This article is purely the author's point of view with regard to the use of languages in the day-to-day official duties of a Tanzanian residing in his home country. Apart from Kiswahili, his national language, the Tanzanian official is faced with another problem: that of having to consult an expatriate officer who does not know Kiswahili on matters of great national interest. In this matter he has at least one alternative: the use of the English language. But Tanzania has invited so many expatriate officers to carry out different national projects. Not all of these expatriate officers are English-speaking; we have French, Germans, Scandinavians, Russians, Chinese, etc., who would like to express their feelings to Tanzanian nationals in their respective native languages.

Is it not true that the use of a native language by its *native speaker* is an indication of what this native speaker really intends to convey to the public concerned? On the other hand is it not true that the use of a native language by a *non-native speaker* may not be an indication of what this non-native speaker really wants to convey to his public? The non-English expatriate officers and surely the Tanzanian nationals themselves, may be victims of this second category. Every time Tanzanians have expressed their feelings about a certain problem by using the English language to English nationals, we have never been fully understood by the native English speakers. As a result, the necessary and immediate action that ought to have been taken thereafter as required by the Tanzanian nationals is often delayed for years! The point has to be clarified again and again for the simple reason that the former wasn't clear enough!

This article suggests only one of the possible ways by which Tanzania and her friends can overcome this crucial problem of *being misunderstood* by one or the other; the adoption of the "Rationale of Translation in Tanzania". This is based on the assumption that if two friendly nations speak different native languages, it is the duty of both nations to learn the native language of the other, so that in times of common crisis, what one nation says about it in its native language is clearly understood by the other friendly nation. This means getting down to *translation work* by both the nations concerned.

As stated earlier, the national language of Tanzania is Kiswahili. The "Rationale of Translation in Tanzania" should, therefore, be from a *foreign language* into Kiswahili and vice versa, for instance: English \rightleftarrows Kiswahili
French \rightleftarrows Kiswahili; Chinese \rightleftarrows Kiswahili; Wolof \rightleftarrows Kiswahili Hausa \rightleftarrows Kiswahili

etc. This type of translation should be encouraged in all our learning institutions including our places of work. It would automatically mean implementing the TANU and Government decision on the use of Kiswahili in the country which was pronounced in 1968.

The type of translation whereby two foreign languages are involved is not advisable in Tanzania for the purpose of large-scale national interests. It trains *nationals* to *think* and *reason* entirely in *foreign languages* about matters of our own national culture. Not only is the information distorted and misunderstood when using these foreign languages to describe our own culture, but also practically not one national of present Tanzania would take heed of the information stated in the foreign languages.

“Ensemble il nous faut cultiver le jardin tanzanien! Le Kiswahili est à la fois un prestige et une identité des indigènes du pays.”